- f) Ulienda shule ya sekondari kwa mda gani? _____
- g) Ulihudhuria chuo kikuu lini? _____
- f) Ulijifunza chuo kikuu kwa mda gani? _____
- h) Ulianza kujifunza kiswahili lini? Kwa nini unajifunza kiswahili? _____
- i) Umejifunza kiswahili kwa mda gani? _____
- k) Utakaa kenya kwa mda gani? _____
- l) Andika juu ya maisha yako _____

ZOEZI LA TATU - EXERCISE THREE.

Use: Ka' Narrative Tense in the following sentences:

1. Mwanalunzi alikwenda ofisini alipata barua.
2. Nialitaka asubuhi, nilioga na nilikunywa chai.
3. Tulijifunza jana usiku tulichoka sana halafu tulilala mapema.
4. Ali alienda sokoni, alinunua mboga na matunda.
5. Matatu ilianguka watu wengi walikufa.
6. Nilienda mjini nilituma barua.
7. Hatukwenda shule; tulikaa nyumbani tulisoma vitabu vingi.
8. Tulifika Malindi saa mbili, tulienda hotelini, tulikula chakula.
9. Tuliona Jack na Jill, tulifurahi sana.
10. Nilienda sokoni, nilinunua matunda, nilimpa Joel moja.

ZOEZI LA NNE: EXERCISE FOUR -

REWRITE THE FOLLOWING SENTENCES USING THE -PO- TENSE:

MFANO - EXAMPLE:

Wakati nilimaliza kula nililala - Nilipomaliza kula nililala

1. Wakati nilitondoka nyumbani wakazi wangu walilia sana.
2. Wakati nilifika Nairobi nilipiga simu Amerika.
3. Nitaturahiti sana wakati nitajua kusema kiswahili.
4. Wakati nitenda soloni nilettee mayai na matunda.
5. Wakati nitapumzika hupenda kusikiliza muziki.
6. Wakati nitasoma sipendi kuongea.
7. Wakati tutamaliza kujifunza kiswahili tutatanya kazi.
8. Wakati nitapata pesa nyingi nitasafiri sana.
9. Nililia sana wakati mama vangu alimandikia barua.
10. Tim aliturahiti sana wakati alipita mtihani.

ZOEZI LA TANO - EXERCISE FIVE

Translate the following sentences into Kiswahili.
Tafsiri sentensi hizi kwa Kiswahili.

1. Before I came to Kenya I was teaching at the University.
2. Yesterday at 3.00 p.m. I was sleeping.
3. When he came in yesterday I was reading a newspaper.
4. Next year I will be working with women's group.
5. Mama was cooking when her friend entered.
6. I was talking to Pete.
7. We were playing basketball.
8. The students were learning how to drive.

MAELEZO YA UTAMADUNI - CULTURAL EXPLANATION:

In much of rural Africa, enquiring about one's age is not at all a sensitive issue. However, western influence is definitely having some impact in this aspect of Kenyan behaviour especially with regards to women.

Unlike Americans Kenyans write the month first then the day and lastly the year i.e. sixth January nineteen ninety five in written as 6/1/95.

BEST COPY AVAILABLE

SOMO LA KUMI NA NNE
PCV/MAMA

UNAFANYA NINI? - WHAT DO YOU DO?

MAZUNGUMZO YA KWANZA - DIALOGUE ONE

PCV: Hujambo Mama?
Mama: Sijambo.
PCV: Habari ya kazi?
Mama: Nzuri kidogo.
PCV: Unaitwaje?
Mama: Ninaitwa Rose. Na wewe je?
PCV: Mimi ninaitwa David.
PCV: Unafanya kazi gani hapa?
Mama: Ninafanya kazi ya biashara.
PCV: Biashara gani?
Mama: Biashara ya Duka.
PCV: Unauza nini?
Mama: Ninauza vyakula tofauti. Na wewe je?
PCV: Mimi ni mshauri wa biashara ndogo.
Mama: Unashauri watu wa biashara gani?
PCV: Ninashauri watu ambao wana biashara ndogo kama wewe.
Mama: Unatoka shirika gani?
PCV: Ninatoka kwa shirika la Peace Corps kutoka Amerika.
Mama: Asante kwaheri tutaonana tena.

MAZUNGUMZO YA PILI - DIALOGUE TWO

John: Hujambo bibi?
Elizabeth: Sijambo. Habari yako?
John: Salama. Labda yako?
Elizabeth: Salama pia.
John: Ninataka kuona daktari, unaweza kunisaidia?
Elizabeth: Ndiyo. Jina lako ni nani?
John: Ninaitwa John Smith. Na wewe je?
Elizabeth: Mimi ni Elizabeth Beach.
John: Nafurahi kukujua Elizabeth.
Elizabeth: Mimi pia. Na unafanya kazi wapi?
John: Mimi ni mwana Peace Corps. Ninafanya kazi pwanj
karibu na kilifi.
Elizabeth: Ah Ndiyo. Nimekumbuka. Wewe ni fundi wa maji?
John: Ndiyo! Lakini kwa sasa ninafundisha vikundi vya
akina mama na shule jinsi ya kutengeneza matanki ya
maji ya mvua na pia usafi wa maji ya kunywa.
Elizabeth: Haya karibu ofisi ya Peace Corps. Daktari hayuko
sasa lakini atarudi saa nane kwa hivyo ngoja kidogo
tu.
John: Asante sana
Elizabeth: Karibu.

READ ALOUD - SOMA KWA SAUTI

Ninafanya kazi. - Sifanyi kazi.
Unafanya kazi. - Hufanyi kazi.
Anafanya kazi. - Hafanyi kazi.

Unafanya nini hapa?
Mimi ni mwanafunzi.
Mimi ni mwalimu.
Mimi ni mkulima.
Mimi ni daktari.
Mimi ni mwanzi biashara.

Mnafanya nini?
Tunajifunza kiswahili.
Tunafundisha Kiingereza.
Tunalima mahindi.

Mimi ni daktari, ninatibu wagonjwa.
Wewe ni mwanafunzi, unajifunza kiswahili.
Yeye ni mkulima, anafuga kuku.
Sisi ni wafanyi biashara, tunauza nguo.
Nyinyi ni wapishi, mnapika chakula.

Kaka yangu hafanyi kazi.
Dada yako hafanyi kazi.
Baba yake amestajafu.

Mimi huenda shuleni.
Wewe huenda chuo kikuu.
Yeye huenda kazini.

Daktari ni mtu ambaye anatibu wagonjwa.

Mkulima ni mtu ambaye analima shamba.
Walimu ni watu ambao wanafundisha.
Wavuvi ni watu ambao huvua samaki.
Mtu ambaye anafundisha.
Mtu anayefundisha.
Watu ambao wanafundisha.
Watu wanaofundisha.
Mtu ambaye.
Watu ambao.

MSAMIATI
SWAHILI

daktari
mvuvi
fundi
mwalimu
mpishi
karanj
mwuguzi
biashara
chuo kikuu

VOCABULARY
PLURAL

madaktari
wavuvi
mafundi
walimu
wapishi
makarani
wauuzi
biashara
vyuo vikuu

ENGLISH EQUIVALENT

doctor
fisherman
technician
teacher
cook
clerk
nurse
business
university

| | | |
|--------------|-----------|--------------|
| shule | shule | school |
| wizara | wizara | ministry |
| shamba | mashamba | farm |
| kikundi | vikundi | group |
| mkulima | wakulima | farmer |
| rais | marais | president |
| hospitali | hospitali | hospital |
| kazi | kazi | work |
| msingi | msingi | foundation |
| staafu(v) | - | retire |
| mwisho | - | last |
| hudhuria (v) | - | attend |
| Elashara | | business |
| kushauri (v) | | advice |
| Shirika | Mashirika | organization |

MAELEZO YA SARUFI - GRAMMAR EXPLANATION:

Amba- is a relative pronoun which when a suffix is added it is equivalent to English 'Who' or 'Which' in a particular noun class
For Example:

M/WA Class

Meaning

Mtu ambaye (sing)
Watu ambao (plu)

The person who...
The people who...

KIVI Class

Kitabu ambacho (sing)
Vitabu ambavyo (plu)

The book which...
The books which...

N Class

Nyumba ambayo (sing)
Nyumba ambazo (plu)

The house which...
The houses which...

Ma Class

Tunda ambalo (sing)
Matunda ambayo (plu)

The fruit which...
The fruits which...

M/MI Class

Mti ambao (sing)
Miti ambayo (plu)

The tree which...
The trees which...

U Class

Ukuta ambao
Kuta ambazo

The wall which...
The walls which...

PA Class

Pahali ambapo (sing)
Pahali ambapo (plu)

The place which...
The places which...

NOTE:

We have the "contracted" forms of the "Amba" pattern which are much more commonly used in daily speech. These "contracted" forms depend upon the use of what we call "relative pronoun markers", which are simply the suffixes that go with "Amba". These are outlined below.

M/WA Class

- YE- (Sing)
- O- (Plu)

KIVI Class

- Cho - (Sing)
- VYO- (Plu)

N Class

-YO- (Sing)
-ZO- (Plu)

MA Class

- LO- (Sing)
- YO- (Plu)

M/MI Class

- O - (Sing)
-YO - (Plu)

U Class

- O - (Sing)
- ZO- (Plu)

PA Class

- PO- (Sing)
- PO- (Plu)

These markers may be used with tense markers NA, LI and TA.
EXAMPLES:

M/WA Class

Mtu anayesoma - Mtu ambaye anasoma (The person who is reading)
Watu wanaosoma - Watu ambao wanasoma (The people who are reading).
Mtu aliyesoma - Watu ambao walisoma (The people who read)
Mtoto atakayekuja - Mtoto ambaye atukuja (The child who will come).
Watoto watakaokuja - Watoto ambao watakuja (The children who will come)

KIVI Class

Kitabu kinachopotea - Kitabu ambacho kinapotea.
(The book which is lost)

Vitabu vinavyopotea - Vitabu ambavyo vinapotea
(The books which are lost).

Kitabu kilichopotea - Kitabu ambacho kilipotea
(The book which got lost).

Vitabu vilivyopotea - Vitabu ambavyo vilipotea
(The books which got lost)

Kitabu kitakachopotea - Kitabu ambacho kita potea
(The books which will get lost)

N Class

Kalamu inayonunuliwa - Kalamu ambayo inanunuliwa
(The pen which is being bought)

Kalamu zinazonunuliwa - Kalamu ambazo zinanunuliwa
(The pens which are being bought)

MA/ Class

Chungwa linalobaki - Chungwa ambalo linabaki
(The orange which is remaining).

Machungwa yanayobaki - Machungwa ambayo yanabaki
(The oranges which are remaining)

M/MI Class

Mti unaoanguka - Mti ambao unaanguka
(The tree which is falling)

Miti inayoanguka - Miti ambayo inaanguka
(The trees which are falling)

Mti ulioanguka - Mti ambao ulianguka
(The tree which fell)

Miti iliyoanguka - Miti ambayo ilianguka
(The trees that fell)

Mmea utakaopandwa - Mmea ambao utapandwa
(The plant which will be planted)

Mimea itakayopandwa - Mimea ambayo itapandwa
(The plants which will be planted)

For more grammar explanation on "Amba" relative pronoun, refer to
your simplified Kiswahili book Page 158 - 170.

In the future continuous, the only change is the future tense marker
-Ta-.

For Example:

| | | |
|-----------------------|---|------------------------|
| Nitakuwa nikijifunza. | - | I will be learning. |
| Utakuwa ukijifunza. | - | You will be learning. |
| Atakuwa akijifunza. | - | S/he will be learning. |

The Negative is as explained above and by following the negation of the future tense -Ta-.

For Example:
Nitakuwa sijifunzi.
Utakuwa hujifunzi.
Atakuwa hajifunzi.

or

Sitakuwa nikijifunza.
Hutakuwa ukijifunza.
Hatakuwa akijifunza.

The Present Perfect Tense -Me- also take the same principle.

For Example:
Nimekuwa nikiishi. - I have been living.
Umekuwa ukiishi. - You have been living.
Amekuwa akiishi. - S/he has been living.

Negation:
Nimekuwa siishi. - I have not been living.
Umekuwa huishi. - You have not been living.
Amekuwa haishi. - S/he has not been living.

or

Sijakuwa nikiishi)
Hujakuwa ukiishi) See above for English meaning
Hajakuwa akiishi)

ZOEZI LA KWANZA - EXERCISE ONE

READING COMPREHENSION

Mzee Juma ana nyumba kubwa na shamba kubwa. Shambani ni kwake nyumbani. Shamba lake lina ekari kumi na tano. Alinunua alipokuwa akifanya kazi ya uwalimu. Kabla ya kuwa mwalimu, alikuwa akifanya kazi ya upandaji miti pamoja na vikundi vya wanawake katika wilaya ya Kakamega. Ana mke na watoto watano. Mtoto wake wa kwanza Shaban, anafanya kazi ya udaktari katika hospitali ya Kenyatta. Mtoto wake wa pili Susan, anafanya kazi ya kupiga chapa katika kampuni ya viatu. Mtoto wa tatu Hamisi, anafanya kazi katika wizara ya maji, yeye ni fundi wa maji. Mtoto wa nne Fatuma, hafanyi kazi anahudhuria chuo kikuu cha Kenyatta. Mtoto wa mwisho Robert, anakwenda shule ya msingi ambayo iko karibu na shamba la baba yake. Mzee Juma alistaafu kazi ya uwalimu alipokuwa na umri wa miaka sitini na tano. Sasa yeye ni mkulima anapanda viazi na kuuza sokoni.

JIBU MASWALI HAYA (ANSWER THE FOLLOWING QUESTIONS)

1. Mzee Juma ana shamba ekari ngapi?
2. Mzee Juma alinunua shamba lake alipokuwa akifanya kazi gani?
3. Mzee Juma ana watoto wangapi?
4. Mzee Juma alistaafu alipokuwa na umri gani?
5. Mtoto wa mzee Juma wa kwanza, hufanya kazi gani?
6. Mtoto wa mzee Juma wa pili anaitwaje na hufanya nini?
7. Mtoto wa mzee Juma wa tatu anafanya nini?
8. Shule ambayo mtoto wa mwisho anahudhuria iko karibu na nini?

ZOEZI LA PILI - EXERCISE TWO:

JIBU MASWALI HAYA (COMPLETE THE FOLLOWING STATEMENTS)
Kamilisha sentensi hizi

1. Mtu ambaye hutibu wagonjwa ni _____.
2. Watu ambao hupika chakula ni _____.
3. Watu wanao vua samaki ni _____.
4. Mtu anayefundisha wanafunzi anaitwaje _____.
5. Fundi ni mtu ambaye hufanya nini? _____.
6. Dereva ni mtu ambaye hufanya nini? _____.
7. Mtu ambaye huendesha ndege huitwaje? _____.
8. Watu ambao hununua na kuuza vitu huitwaje? _____.
9. Karani ni mtu ambaye hufanya nini? _____.
10. Rais ni mtu ambaye hufanya kazi gani? _____.

ZOEZI LA TATU - EXERCISE THREE:

JAZA KATIKA NAFASI UKITUMIA "AMBA" (FILL IN THE BLANKS USING AMBA
RELATIVE PRONOUNS)

FOR EXAMPLE

Mtu _____ anasoma ni kaka yangu. = Mtu ambaye anasoma ni kaka yangu.

1. Yule mtu _____ anazungumza nje ni rafiki yangu.
2. Watoto _____ watakwenda lamu ni wanafunzi.
3. Ali ni mtu _____ alisomea ng'ambo kwa chuo kikuu.
4. Niliwaona watu _____ walikuwa dukani.
5. Wanafunzi _____ wanakatazwa kutoka nje ni wasichana.
6. Kitabu _____ alisoma kilipotea jana usiku.
7. Waliambiwa waukate mti _____ unakabiliana na nyumba yetu.
8. Tafadhali mpe Jim kalamu _____ nilikupa jana jioni.
9. Nyumba hizi zilijengwa pahali _____ hakuna watu wengi.
10. Machungwa _____ nilinunua sokoni hayakuwa mazuri sana, yalikuwa yameoza.

ZOFZI LA NNE - EXERCISE FOUR

CONVERT THE FOLLOWING SENTENCES BY USING CONTRACTED FORMS OF 'AMBA'.

For Example:

Mtu ambaye anasoma kitabu ni rafiki yangu.
Mtu anayesoma kitabu ni rafiki yangu.

1. Mwanapisko ni mtu ambaye husaidia watu.
2. Walimu ni watu ambao wanafanya kazi ya kufundisha.
3. Viatu ambavyo vilipotea ni vya mwanafunzi.
4. Kitabu ambacho tunasoma ni cha kiswahili.
5. Nguo ambazo alivaa zilikuwa chafu.
6. Ndizi ambayo alinipa ni mbaya.
7. Barua ambayo ulituma ilifika.
8. Haya ni machungwa ambayo ulinituma.
9. Mtu ambaye alikuwa Raisa wa Kenya ni nani?.
10. Njia ambayo nilifuata ni ndefu sana.
11. Kazi ambayo nilifanya Amerika ni nzuri.
12. Watu ambao wanaishi Amerika wanaitwaje?.

Cultural Note:

Work is something you do and you are paid for or get some income from it e.g. a housewife cannot say she is working.

SOMO LA KUMI NA TANO

IKO WAPI? - WHERE IS IT?

MAZOEZI YA UFAHAMU: COMPREHENSION EXERCISE.

MJI WA NAIVASHA.

Naivasha ni mji mdogo. Uko kaskazini magharibi ya Nairobi. Ni mji ambao umezungukwa na mashamba ya wakulima wengi. Watu wengi wanaoishi Naivasha ni wafanyi biashara. Wanauza nguo, vyakula na vitabu. Maduka mengi ni ya rejareja na mengine ni ya jumla. Kuna vituo vya petroli, posta, benki na hospitali. Viwanda ni vichache tu. Kuna kiwanda cha kukausha mboga, kiwanda cha maziwa na kiwanda cha mvinyo wa Rumika. Viwanda hivi vimeajiri watu wengi.

Upande wa kusini ya Naivasha kuna ziwa la Naivasha. Kuna mashamba kando ya ziwa. Pia, huku wakulima wanakuza vyakula kama maharagwe, viazi, matunda kama kabibu, machungwa na mboga. Wakulima hawa wanatumia kilimo cha hali ya juu kwa sababu wananyunyizia maji kutoka ziwani. Vyakula vingi hutumwa nchi za nje. Wakulima wengine hupanda maua ambayo hutumika Nairobi, na mengine hutumwa nchi za nje ili kupatia Kenya pesa za kigeni.

Mashariki na Magharibi ya Naivasha ni kavu. Hapo mifugo kama mbuzi, kondoo, ngombe wa nyama na wa maziwa hustawi sana. Kaskazini zaidi kuna milima ya Nyandarua. Hapa kuna mbuga za wanyama na msitu pia. Watalii wengi hupitia hapa wanapoenda kuona wanyama, misitu na pia wanapoenda Hotel kubwa ambazo ziko karibu na ziwa la Naivasha.

SOMA KWA SAUTI - READ ALOUD.

Niko darasani. - Tuko darasani.
Uko ofisini. - Mko ofisini.
Yuko kazini. - Wako kazini.

Mwalimu yuko wapi? Nwalimu yuko darasani anafundisha.
Mama yuko wapi? Mama yuko jikoni anapika ugali.
Wanafunzi wako wapi? Wanafunzi wako darasani.

Kitabu kiko Juu ya meza, chini ya meza.
Vitabu viko

Kikombe kiko Kabatini, ndani ya kabati.
Vikombe viko

Saa iko wapi? Chumbani, dukani.
Taa ziko wapi? Iko dukani.

Ezekiel yuko nyumbani? La hayuko nyumbani.
Yuko mjini.

| | |
|--|--|
| | La hayuko nyumbani, Yuko kazini. |
| | La hayuko nyumbani. Yuko darasani. |
| Choo kiko wapi? | Choo kiko nyuma ya atisi. Choo kiko karibu na baa. Choo kiko ndani ya nyumba. |
| Posta iko wapi? | Posta iko katika barabara ya Moi. Iko mbele ya stesheni ya basi. Iko karibu na soko. |
| Kenya Iko wapi? | Iko Afrika Mashariki. Nairobi iko katikati ya Kenya. Uganda iko magharibi ya Kenya. Tanzania iko kusini ya Kenya. Ethiopia iko kaskazini ya Kenya. |
| Mwaka uliopita ulikuwa wapi? | Nilikuwa Amerika. Nilikuwa Chuo kikuu. |
| Kesho utakuwa wapi? | Nitakuwa darasani. Nitakuwa mjini. Nitakuwa Nairobi. |
| Jana usiku ulikwa wapi? Mwenye kiti alikuwako? Mpishi yuko kazini leo? | Nilikuwa mkutanoni. Hapana, hakuwako. Hapana hayuko, Ndio yuko jikoni. |

MSAMIATI

juu ya
chini ya
mbele ya
nyuma ya
ndani ya
nje ya
kati ya / Katikati ya
baina ya
zaidi ya
badala ya
karibu na/ va
mbali na
pamoja na
ngambo ya
magharibi
mashariki
kusini
kaskazini
posta
benki
choo

VOCABULARY

on top of / Above/ About
underneath, below
in front of
behind
in / Inside
out of / Outside of
in the middle of / in the midst of
between / in between
more than, in addition to
instead of
near to / near
far From
with, together with
across
west
east
south
north
post office
bank
toilet

| | |
|---------------------------|-------------------------|
| ofisi | office |
| daraja | bridge |
| soko | market |
| mto | river |
| mlima | mountain |
| bahari | ocean |
| kituo cha Polisi | police station |
| kituo cha basi | bus station |
| njia | road/path/way |
| kuelekeza | to guide |
| simu (N) | telephone |
| kama | about / If |
| umbali (N) | distance |
| kanisa (N) | church |
| kilima (N) | hill |
| kivuko (N) | ferry |
| kuvuka (N) | to cross |
| njia Panda (N) | fork road |
| makutano ya Njia/barabara | crossroads |
| mzunguko wa barabara | roundabout |
| kituo (N) | station / stop / centre |
| kukabili | to face |
| kuajiri (V) | to employ |
| kustawi | to prosper |
| pesa za kigeni | foreign exchange |

MAELEZO YA SARUFI - GRAMMAR EXPLANATION

The Locative verb -Ko- /P and -Mo-. In Swahili the locative verbs equivalent to English "Is" and "Are" is denoted by the following:

- 1) -Ko- suffix which shows an indefinite place in M-WA Noun class, we get:-
- | | | | |
|--------|---------|---|-----------------|
| Niko - | I am |) | |
| Uko - | You are |) | Positive Plural |
| Yuko - | S/he is |) | |

In negation, only the subject prefix changes to negative subject prefix.

For Example:

| | | | | |
|--------|---|--------------|---|-------------------|
| Siko | - | I am not |) | |
| Huko | - | You are not |) | Negative singular |
| Hatuko | - | They are not |) | |

Negative plurals are formed prefixing the negative prefixes to the locative -Ko-.

Note:

That the other locative forms -Po- which is for a define place and -Mo- which denotes insideness follow the same pattern as above. However they are not as widely used as -Ko- locative and hence we do not go into details at this stage.

It is important to note that the locative -ko- is only used in the present tense for past and future tenses. The verb to be 'KUWA' in it's locative form is used:

For example: In the past tense

| | | |
|-------------------------|---|-----------------------------|
| Jana nilikuwa nyumbani. | - | Yesterday I was at home. |
| Jana ulikuwa nyumbani. | - | Yesterday you were at home. |
| Jana alikuwa nyumbani. | - | Yesterday s/he was at home. |

And in the Future:

| | | |
|-------------------------|---|-----------------------------------|
| Kesho nitakuwa Nairobi. | - | Tomorrow I will be in Nairobi. |
| Kesho utakuwa Nairobi. | - | Tomorrow you will be in Nairobi. |
| Kesho atakuwa Nairobi. | - | Tomorrow S/he will be in Nairobi. |

All the above examples are in M-WA Class only for other noun classes, the subject prefixes are used as in all the other verb tenses covered.

There is a very useful suffix which can be added to almost any common noun (except Human and Animals) to denote the meaning of in, on, at, near, by, etc. This suffix is -ni.

For Example:

| | | | |
|--------|----------|---|-----------------|
| Jiko | Jikoni | - | In the kitchen. |
| Mkono | Mkononi | - | In the hand. |
| Soko | Sokoni | - | At the market. |
| Duka | Dukani | - | At the shop. |
| Meza | Mezani | - | On the table. |
| Nyumba | Nyumbani | - | At home. |
| Mji | Mjini | - | In town. |
| Kazi | Kazini | - | At work. |
| Mfuko | Mfukoni | - | In the pocket |
| Ofisi | Ofisini | - | In the office |

ZOEZI LA KWANZA - EXERCISE ONE

Read the pasage again and answer the following questions.

1. Mji wa Naivasha uko upande gani kutoka Nairobi?
2. Ni mimea gani hukuzwa kando ya ziwa?
3. Taja kazi mbili ambazo watu wanafanya Naivasha
4. Kuna viwanda gani katika Naivasha?
5. Watu wa Naivasha wanauza maua ya wapi?
6. Kwe nini nchi ya Kenya huuza vitu vyao katika nchi za nje?
7. Milima gani iko kazkazini ya Naivasha?
8. Kuna nini huko karibu na miima?
9. Upande gani wa Naivasha ni mkavu? Watu hufanya nini?

ZOEZI LA PILI - EXERCISE TWO:

REWRITE THESE SENTENCES - AFFIRMATIVE TO NEGATIVE AND VISE VERSA.

1. Watoto wako darasani.
2. Jana mpishi alikuwa jikoni.
3. Posta iko karibu na banki ya Barclays.
4. Vikombe haviko kibatini.
5. Mama hayuko sokoni.
6. Chakula hakiko tayari.
7. Jacob alikuwa katika mkutano.
8. Kesho sitakuwa darasani.
9. Jumatatano mtakuwa Nairobi.
10. Mji wa Naivasha uko katika mkoa wa Rift Valley.
11. Jana nilikuwa kazini.
12. Pesa zangu ziko benki.
13. Barua zako ziko posta.
14. Nancy hayuko kazini leo, yuko nyumbani.
15. Sikuwa mjini jana usiku.
16. Kesho tutakuwa mkutanoni Nairobi.

ZOEZI LA TATU - EXERCISE THREE

FROM THE WORDS IN THE BRACKETS, CHOOSE THE CORRECT FORM OF THE LOCATIVE KO. COMPLETE THE SENTENCES:

1. Kitabu (mko, ako, kiko) kibatini.
2. Mwalimu (wako, kiko, yuko) wapi?.
3. Pesa zangu (yuko, ziko, viko) katika kibeti.
4. Kesho (niko, nilikuwa, nitakuwa) kazini.
5. Posta (viko, iko, niko) wapi?.
6. Kituo cha basi (liko, yuko, kiko) karibu na soko.
7. Jana (uko, umekuwa, ulikuwa) wapi?.
8. Wanafunzi (yako, liko, wako) darasani?.
9. Chakula (hayuko, hakiko, haliko) tayari.
10. Wikendi ijayo (hamtakuwa, havitakuwa, hayatakuwa) Naivasha, mtakuwa Nairobi.

BEST COPY AVAILABLE

SOMO LA KUMI NA SITA

KUULIZA NJIA - ASKING FOR DIRECTIONS

MAZUNGUMZO YA KWANZA - DIALOGUE 1

Ruth: Hujambo bwana?
Njire: Sijambo, habari yako?
Ruth: Nzuri, labda yako?
Njire: Nzuri pia.
Ruth: Unaweza kunisaidia tafadhali? Mimi ni mgeni hapa, na ninatafuta kituo cha Polisi. Tafadhali nionyeshe njia ya kwenda huko.
Njire: Unataka kwenda Polisi?
Ruth: Ndiyo, tafadhali.
Njire: Una shida gani?
Ruth: Ni mwizi ameiba saa na pesa zangu.
Njire: Oo! Pole, haya kwenda Polisi, utafuata njia hii moja kwa moja, ukifika karibu na ofisi za D.O. piga kona, mbele utaona mlima mdogo, panda huo mlima, pinda kushoto na utaona kituo cha Polisi mbele yako upande wa kulia wa barabara.
Ruth: Haya, asante sana.
Njire: Kwaheri ya kuonana.
Ruth: Kwaheri.

MAZUNGUMZO YA PILI - DIALOGUE 2

Kimani: Hujambo bwana?
John: Sijambo, habari gani?
Kimani: Salama sana. Mimi naitwa Kimani.
John: Jina langu ni John.
Kimani: Nafurahi kukujua John.
John: Mimi pia nafurahi kukutana na wewe.
Kimani: Nina shida kidogo sijui kama unaweza kunisaidia?
John: Shida gani?
Kimani: Ninatafuta chuo cha mafunzo cha Peace Corps.
John: Ninajua kiko hapa Naivasha lakini sijui ni wapi?
Kimani: Oo! Pahali kuna waamerika wengi?
John: Ndiyo! Hapo.
John: Ni karibu na shule ya wasichana ya Naivasha.
Kimani: Sijui hiyo iko wapi pia.
John: Unaona barabara hii?
Kimani: Ndiyo.
John: Ifuate mpaka pale kwa kona ya "Multiline" halafu kata kushoto. Fuata hiyo barabara moja kwa moja, pita steji ya Matatu na baada ya kupita kidogo tu utaona makutano ya barabara. Hapo kata kulia katika barabara ya Mama Ngina.
Kimani: Barabara ya Mama Ngina?

John: Adiyo, ifuate mpaka kwa kona, halafu kata
kushoto na utaona ofisi za mkuu wa taarafa ya Naivasha.
Enda moja kwa moja panda miima mdogo na pinda kulia.
Fuata barabara hiyo. Utapita nyumba nyingi mkono wa
kushoto na mbele utaona kibao cha kituo cha mafunzo
ya Wana Peace Corps upande wa kulia.

Kimani: Asante sana bwana, ninashukuru.
John: Karibu bwana.
Kimani: Haya, kwaheri.

SOMA KWA SAUTI READ ALOUD

Nenda moja kwa moja.
Enda moja kwa moja.
Fuata barabara hii.
Fuata barabara hiyo.
Pinda kushoto.
Kata kulia.
Fuata njia hii moja kwa moja.
Enda kushoto.
Enda kulia.

Pita Posta na Benki.
Ukiona Benki pinda kushoto.
Ukipita shule kata kulia.
Ukipita daraja enda kidogo.
Halafu pinda kulia.
Ukifuata barabara hii utafika hapo.
Utakapoona shule kata kushoto.
Shule iko karibu na msitu.
Duka liko mbele ya kanisa.
Kanisa liko juu ya kilima.
Utaenda kidogo tu.
Ukifuata barabara ya Kenyatta utaona Benki upande wa kushoto.
Nitaona nini?
Utaona Posta.
Utaona Benki kushoto.
Utapita daraja.
Utafika makutano ya barabara.
Ukifika utaona mzunguko.
Pita mzunguko.
Utaona chuo cha Waalimu.

MSAMIATI

Nionyeshe
Fuata (V)
Pinda (V)
Kata (V)
Niambie (V)
Ramani (N)

MISAMIATI

tuonyeshe

tuambie
ramani

VOCABULARY

show me
follow
turn
cut / turn
tell me
map

| | | |
|---------------|----------|----------------|
| Onyesha (V) | | show |
| Upande (N) | pande | side/direction |
| Upande wa | pande za | side of |
| kulia | | right |
| kushoto | | left |
| mkono | | hand/arm |
| endelea | | continue |
| moja kwa moja | | straight |
| pita | | pass |
| weza | | be able |
| ona | | see |
| teremka (V) | | go down |
| panda (V) | | climb |
| uliza (V) | | ask |
| saidia (V) | | help |
| mbele (PRP) | | front/infront |
| angalia (V) | | look |

MAELEZO YA SARUFI - GRAMMAR EXPLANATION:

The conditional Tense -Ki-
In Swahili the conditional tense equivalent to English "If" is -Ki-
It is formed like other tenses by being after the subject prefix:

For Example:

| | | |
|----------|---|------------------|
| Nikienda | - | If I will go. |
| Ukienda | - | If you will go. |
| Akienda | - | If S/he will go. |

The plurals are formed by prefixing the plural subject prefixes.

-Sipo-

For Example:

| | | |
|------------|---|----------------------|
| Nisipoenda | - | If I will not go. |
| Usipoenda | - | If you will not go. |
| Asipoenda | - | Is S/he will not go. |

Negative Plurals:

| | | |
|------------|---|----------------------|
| Tusipoenda | - | If we will not go. |
| Msipoenda | - | If you will not go. |
| Wasipoenda | - | If they will not go. |

Note: That the -Ki- tense is used in place of it's long form "Kuwa" which literary means "If it Be".

The Imperative Verb:

The imperative form of the verb is formed by dropping the infinitive -Ku- in polysyllabus verbs but retains the infinitive in monosyllabus verbs.

For Example:

| | | | |
|------------|---------|---|-------------|
| (Ku)sema | Sema! | - | Speak! |
| (Fu)andika | Andika! | - | Write! |
| (Ku)soma | Soma! | - | Read! |
| (Ku)enda | Enda! | - | Go! |
| (Ku)fuata | Fuata! | - | Follow! |
| (Ku)ona | Ona! | - | See! |
| (Ku)fika | Fika! | - | Arrive etc. |

Note that imperatives in swahili could be commands or requests, this is indicated by the tone of voice used.

In plural formation the suffix -Eni- is placed at the end of the imperative for verbs ending with vowel. -N- and -Ni- for verbs end in -O- or -U- which are derived from Arabic.

For Example:

| Singular | | Plurals | |
|----------|---|----------|-------------------------|
| Sema | - | Semeni | - You (plural) speak. |
| Andika | - | Andikeni | - You (plural) write. |
| Soma | - | Someni | - You (plural) read. |
| | | and | |
| Njoo | - | Njoo ni | - You (plural) come. |
| Abudu | - | Abuduni | - You (plural) worship. |

The negative of the imperative is formed putting together the subject prefix of the second person U in singular and M in the plural before the verb stem and changing the final vowel A to E

For Example:

| | | | | |
|----------|---|-----------|---|-------------------------------|
| Sema | - | Usieme | - | Do not speak. |
| Andika | - | Ustandike | - | Do not write. |
| Andikeni | - | Mstandike | - | You (plural) do not write. |
| Someni | - | Msisome | - | You (plural) do not read etc. |

For more details please refer to simplified Swahili page 8.

ZOEZI LA KWANZA : EXERCISE ONE

EXAMPLE: Fuata - Fuatani
Jaribu - Jaribuni

Change the Verbs in brackets to their imperative or subjunctive forms.

Example: Alisema ____ (ona) baada ya kazi.
Alisema nimuone baada ya kazi.

1. Aliniambia _____ (kupa) pesa za chakula.
2. Alimwambia _____ (kuja) jioni ya leo.
3. Tulienda mjini ili _____ (kuona) rafiki yetu.
4. " _____ (keti) hapo ! alisema kwa sauti kubwa.

5. _____ (kusoma) kitabu hiki! mwalimu alimwambia mwanafunzi.
6. "_____ (kupika) chakula cha jioni" mama aliamuru mtoto.
7. _____ (kutafuta) kalamu yangu.
8. "_____ (kukaa) hapa mpaka nirudi" mama alimwambia mtoto.
9. Nilisema _____ (kupika) chai!
10. Polisi alipomwona mwizi alimwambia _____ (kusimama) haraka sana.

ZOEZI LA PILI - EXERCISE TWO

TAFSIRI KWA KISWAHILI - TRANSLATE INTO SWAHILI.

1. Please show me the way to Barclays's Bank.
2. Show him the way to the Post Office.
3. Go straight, then turn left at the corner.
1. The market is behind the Bus Station.
5. If you follow this road you will see the Police Station on your right.
6. I asked him to show me the way to your office.
7. Please ask that man the way to the movie theatre.
8. Where is the Bus Stage from here?
9. Where is the Peace Corps Office in Nairobi?
10. Please direct me to the market.

ZOEZI LA TATU - EXERCISE THREE

The following sentences are written in the long form of the future conditional tense: "Ikiwa/Kama. Please Change them to the contracted form "-Ki/Sipo". Use a separate paper.

1. Ikiwa nitafuata njia hii, nitafika Posta?
2. Nitafika shule ya sekondari ikiwa nitapita hapa.
3. Tutapitia wapi ikiwa tunataka kufika haraka.
4. Ikiwa ninataka kwenda Malaika nitahitaji kupanda matatu.
5. Kama nitenda mjini kwa miguu nitapitia njia ya mkato.
6. Ikiwa utienda Posta pitia Benki unilettee pesa.
7. Ikiwa utamwona Mary mwambie apitie dukani anunue vyakula.
8. Ikiwa hutafuata barabara hii utapotea.
9. Ikiwa mwalimu atapotea njia hatutajifunza kiswahili.
10. Ikiwa utachelewa mjini utapotea njia ya kwenda nyumbani usiku.

CULTURAL NOTES:

- a) In Kenyan culture, unlike Western culture, directions are usually given using land marks for example a bridge, a river or, a big tree, a building. Thus it is rare to hear kenyans using names of streets, roads and numbers when giving directions to a place.
- b) Although it varies with particular ethnic groups, distance could be shown to be nearer or farther than in actual kilometers. Please clarify this area with your language teacher(s) and compare differences.

SOMO LA KUMI NA SABA

KUNUNUA TIKITI - BUYING A TICKET

MAZUNGUMZO YA KWANZA - DIALOGUE ONE.

Tom: Habari gani Karani?
Karani: Salama tu
Tom: Ninataka kwenda Mombasa kwa basi.
Ninaweza kupata tikiti?
Karani: Ndio. Unataka kusafiri lini?
Tom: Jumamosi kuna basi ngapi?
Karani: Mbili tu. Moja linaondoka saa
saba mchana na lingine linaondoka saa mbili usiku.
Tom: Basi ya mchana hufika Mombasa saa ngapi?
Karani: Hufika saa tatu usiku.
Tom: Kuna nafasi katika basi hilo?
Karani: Ndio kuna nafasi.
Tom: Nauli ya kwenda ni shilingi ngapi?
Karani: Ni shilingi mia mbili.
Tom: Nipe tikiti moja ya mtu-mzima.
Hizi shilingi mia mbili.
Karani: Haya bwana chukua tikiti yako. Una mizigo?
Tom: Ndiyo nina mizigo mmoja mdogo.
Karani: Haya fika hapa nusu saa kabla ya wakati wa kuondoka.
Tom: Haya, Asante.

MAZUNGUMZO YA PILI - DIALOGUE TWO.

Ben: Vipi bwana?
Ken: Salama tu ninaweza kukusaidia?
Ben: Ndio. Ninataka kununua tikiti ya kwenda Machakos.
Ken: Ungetaka kusafiri lini?
Ben: Kesho, saa mbili.
Ken: Pole Bwana, Basi la kwanza limejaa lakini kuna nafasi.
Katika basi la pili. Unaweza kusafiri saa nane?
Ben: Sawa tu. Hakuna shida. Ni pesa ngapi kwenda tu?
Ken: Ni shilingi mia moja.
Ben: Ninaweza kupata kiti cha nyuma karibu na dirisha.
Ken: Ndio. Una mizigo?
Ben: Ndio. Miuko mmoja tu.
Ken: Basi, jaribu kuwa hapa kesho kabla ya saa nane.
Ben: Haya, kwaheri tutaonana kesho.

MAZUNGUMZO YA TATU - DIALOGUE THREE:

KUSAFIRI KWA MATATU

Manamba: Habari gani? Unaenda?
Msafiri: Ndiyo ninaenda lakini nitaketi wapi?
Manamba: Kuna nafasi njoo utapata kiti.
Msafiri: Wapi nafasi? Na watu wamejaa?
Nitaketi wapi? Na sitaki kusimama.
Manamba: Njoo kuna nafasi ya watu wawili.
Njoo nitakutafutia kiti. (katika matatu)
Haya songa mpaka mwisho. Hapa kuna nafasi ya watu
wawili. Kaa kibiashara.
Msafiri: Songeni tafadhali sijaketi vizuri.
Manamba: Haya kila mtu lipa pesa yako tunaondoka sasa.

SOMA KWA SAUTI - READ ALOUD

Basi huondoka saa ngapi? Basi huondoka saa mbili.
Basi huondoka saa tano.
Basi huondoka saa nane.

Matatu husafiri kwa muda gani?
Matatu huchukua muda wa saa moja.
Matatu huchukua muda wa masaa mawili.

Basi husimama Voi kwa muda gani?
Basi husimama Voi kwa dakika ishirini.
Matatu husimama Voi kwa masaa mawili.

Matatu husafiri moja kwa moja, au husimama - simama njiani?
Matatu husimama Naivasha.
Matatu husimamasimama njiani.
Matatu itaenda moja kwa moja.

Nauli ya kwenda ni shilingi ngapi?
Nauli ya kwenda ni shilingi hamsini.
Nauli ya kwenda na kurudi ni shilingi mia.

Tikiti ni pesa ngapi? Tikiti ni shilingi mia tatu.
Tikiti ni shilingi arobaini.
Tikiti ni shilingi sabini.

Una mizigo mingapi? Nina mizigo mingi.
Nina mgigo mmoja.
Sina mzigo.

Ninaweza kuketi karibu na dirisha?
Ndio unaweza.
La huwezi, hakuna nafasi.

Ningependa kununua tikiti ya kwenda na kurudi.
 Ningetaka kununua tikiti ya kurudi tu.
 Ningetaka kununua/tikiti ya watu wawili.
 Ningependa kusafiri mchana / usiku.
 Ungependa kuketi wapi?
 Karibu na mlango.
 Basi hili limejaa, siwezi kulipanda.
 Kituo cha gari la moshi kiko wapi?
 Mwisho wa barabara hii.
 Basi litaondoka saa ngapi?
 Saa tatu asubuhi.
 Kuna nafasi?
 Ndio kuna nafasi.
 Matatu imejaa.
 Basi halijajaa.
 Hakuna nafasi.

MSAMIATI

tikiti
 nauli
 abiria
 kusimama
 kuwasili/kufika
 -ingine
 -ngapi
 barabara
 kiti cha mbele
 kiti cha nyuma
 kiti cha katikati
 karibu na dirisha
 kwa basi
 kwa Ndege
 kulipa
 kujaa
 songa
 manamba
 kwa Matatu
 kiti
 njia
 ondoka
 mchana
 mzigo
 chukua
 pesa
 pata
 saa
 safari
 safiri
 simama
 tembea
 nafasi

VOCABULARY

ticket
 fare
 passenger
 to stop
 to arrive
 other
 how many
 way / road/ path
 front seat/chair
 back seat/chair
 middle seat/chair
 near the window
 by bus
 by airplane
 to pay
 to be full
 move
 tout
 by matatu
 chair / seat
 way / path
 leave
 afternoon
 luggage/load
 take
 money
 get
 time
 trip/journey
 travel
 stop
 walk
 space

ZOEZI LA KWANZA - EXERCISE ONE

'ME' AND 'HU' TENSE

TAFSIRI SENTENSI HIZI - TRANSLATE THIS SENTENCES:

1. Basi imejaa; Hakuna nafasi.
2. Gari la moshi huondoka saa moja ya asubuhi.
3. Watu husafiri vipi kwenda nyumbani.
4. Ncege huchukua muda gani kutoka New York Mpaka Nairobi.
5. Nimechoka sana kwa sababu ya safari hiyo.
6. Mwalimu yule amekasirika kwa sababu nimechelewa.
7. Chakula chako ni kizuri, nimeshiba sana.
8. Watoto wamelala kwa sababu wamechoka.
9. Wanafunzi wamekasirika kwa sababu hakuna Mwalimu.
10. Ametafuta njia lakini hajarona.
11. Mzee yule amekufa kwa sababu ya uzee.
12. Kama umemaliza mtihani, pumzika kidogo.
13. Amejifunza lugha kwa muda.
14. Mkutano huanza saa mbili.
15. Mimi huenda Nairobi mara mbili kwa wiki.
16. Mayai hupatikana sokoni tu.
17. Mtu anapoumwa na tumbo humeza dawa hii.
18. Kwa kawaida mvua hunyesha mwezi wa Machi.
19. Nyinyi hupenda kusafiri vipi?
20. Maji huingia mfereji gani??

ZOEZI LA PILI - EXERCISE TWO:

JIBU MASWALI HAYA.

1. Unakaa wapi?
2. Wewe husafiri vipi kwenda nyumbani?
3. Wewe hulipa pesa ngapi kwa matatu kutoka Naivasha kwenda nyumbani.
4. Matatu huondoka saa ngapi kwenda nyumbani?
5. Wewe hufika Malaika saa ngapi?
6. Unapenda kusafiri kwa Matatu? Eleza.
7. Hapa nchini, watu husafiri vipi?
8. Je, umewahi kusafiri kwenda mbali? Eleza juu ya safari yako.

ZOEZI LA TATU - EXERCISE THREE:

TAFSIRI SENTENSI HIZI - TRANSLATE THE FOLLOWING SENTENCES.

1. I don't like travelling at night.
2. Travelling by bus is better than travelling by Matatu.
3. How do you like travelling?
4. Is the bus full?
5. The bus is full, there's no space.
6. The train goes to Nairobi twice a week.
7. I have finished packing my luggage. You can put it on the bus now.
8. How long does a plane take from New York to Nairobi?.
9. When will the bus depart?
10. I always go to Nairobi by Matatu.
11. Usually it rains during the month of March.

ZOEZI LA 4 - EXERCISE FOUR.

TAFSIRI SENTENCSI HIZI - TRANSLATE THE FOLLOWING SENTENCES.

1. Basi limejaa, hakuna nafasi.
2. Nauli ya kwenda na kurudi ni pesa ngapi?
3. Ningetaka kuketi karibu na dirisha.
4. Basi litaondoka saa ngapi?
5. Matatu huchukua muda gani kutoka Nairobi hadi Naivasha?
6. Ninataka kununua tikiti za watu wanne.
7. Wewe husafiri vipi kwenda nyumbani?
8. Gari la moshi limeondoka.
9. Ndege huchukua masaa mangapi kutoka N.Y. mpaka Nairobi.
10. Ninapenda kusafiri usiku.

CULTURAL NOTE:

"A Matatu is never full." Even if it's full, the Manambas (Touts) will always push people to get in.

- In Kenya people travel with their luggage in the same vehicles.
- At times when you go to a bus stage the touts (Manambas) will run to you, grab your luggage and take it to their respective vehicles expecting you to follow them. Watch out!
- You may find a matatu which you think is almost full and that will be the first to leave. Don't be suprised when it turns out that most of the "passengers" were Manambas trying to fool travellers. However, long distance Matatus line up and leave one after the other.

Usually there is no personal space in public transport.

SOMO LA KUMI NA NANE

HALI YA HEWA NI VIPI? - HOW IS THE WEATHER?

SOMA KWA SAUTI - READ ALOUD

Leo hali ya hewa ni vipi?
Leo kuna baridi.
Leo kuna joto.
Leo kuna mvua.
Leo kuna manyonyu.
Leo kuna upepo.
Mvua inanyesha.
Mvua hainyeshi.
Jana mvua ilinyesha.
Jana mvua haitanyesha.
Kesho mvua itanyesha.
Kesho mvua haitanyesha.
Kuna upepo / vumbi leo.
Hakuna upepo.
Kuna joto jingi.
Hakuna joto jingi.
Kuna mvua nyingi.
Hakuna mvua nyingi.
Leo hali ya hewa ni nzuri.
Leo hali ya hewa ni mbaya.
Ninasikia joto sana.
Ninasikia baridi sana.
Ninasikia baridi kidogo.
Habari za nyumbani?
Nzuri lakini kuna ukame.
Nzuri, mvua inanyesha kidogo.
Wakulima wanapanda vyakula vingi.
Kuna baridi, wakulima hawapandi vyakula.
Majira.
Majira ya kiangazi.
Majira ya masika.
Majira ya vuli.
Majira ya baridi.
Katika majira ya kiangazi kuna nini?
Majira ya kiangazi kuna joto jingi na jua kali.
Majira ya masika kuna nini.
Majira ya masika kuna mawingu mengi na mvua nyingi.
Majira ya vuli kuna nini?
Majira ya vuli kuna joto kidogo na upepo.
Majira ya baridi kuna nini?
Majira ya baridi kuna baridi nyingi na umande mwingi wakati wa asubuhi.

MSAMIATI
Swahili

majira
kiangazi
masika
vuli
baridi sana
mvua
mawingu
aina
manyunyu
upepo
jua
kusikia
joto
baridi
kunyeshha
kuvuna
kufurahi
ukame
hali ya hewa
kwa kawaida
jimbo
mkulima
mazao
mpaka

VOCABULARY
ENGLISH

season
hot season
rainy season
season of lesser rains
cold season
rain
clouds
type
drizzling (of rain)
wind
sun
to feel
hot and humid
cold
to rain
to harvest
to be happy
drought
weather
usually
state
farmer
crops/produce
up until

READING COMPREHENSION

Katika nchi ya Kenya, kuna majira ya masika, kiangazi na vuli. Hakuna majira ya kipupwe lakini kuna majira ya baridi.

Kwa kawaida, majira ya kiangazi huanza mwenzii wa Disemba na huendelea mpaka machi. Katika majira ya kiangazi, kuna joto jingi na jua kali.

Majira ya masika huanza mwenzii wa machi au April. Mvua hunyeshha sana katika majira haya. Wakulima hufurahi sana katika majira haya, kwa sababu katika majira haya, huweza kupanda vyakula vya aina nyingi.

Majira ya baridi huanza mwisho wa mwezi wa sita na huendelea mpaka mwezi wa tisa. Wakati huu, wakulima hawafanyi kazi shambani. Kwa hivyo vyakula huwa bei ghali sana. Na katika majira ya vuli kuna joto kidogo na upepo. Vuli ni majira ya kuvuna vyakula. Wakulima hufurahi sana. Mazao mengi, kama ndizi, mihogo, viazi na matunda mengi, hupatikana katika majira haya.

MAELEZO YA SARUFI - GRAMMAR EXPLANATION.

In this lesson we have used adjectives like -ingi, -baya and -zuri. In Kiswahili, adjectives come in three categories.

PREFIX - DEPENDANT ADJECTIVES BEGINNING WITH A CONSONANT

| | |
|---------|---|
| -zuri | good |
| -baya | bad |
| -bichi | raw, unripe, uncooked |
| -bivu | ripe |
| -chache | few |
| -chafu | dirty |
| -changa | young |
| -chungu | bitter |
| -dogo | small, little |
| -fupi | short |
| -geni | strange, foreign |
| -gumu | hard, tough, difficult |
| -janja | cunning, clever, deceitful |
| -jinga | foolish, ignorant, stupid |
| -kali | fierce, sharp, strict, strong |
| -kubwa | big, large, main |
| -kuu | great, chief |
| -kukuu | old, wornout |
| -moja | one |
| -nane | eight |
| -ngapi? | how many |
| -nne | four |
| -nono | fat (animals) |
| -nene | stout, fat (people) |
| -nyonge | weak, poor, feeble, unhealthy |
| -pana | broad, wide |
| -pole | gentle (often used as the opposite of kali) |
| -mpya | new, fresh |
| -refu | tall, long, high |
| -tamu | sweet |
| -tano | five |
| -tatu | three |
| -tupu | empty, bare |
| -tulivu | peaceful, calm |
| -wili | two |
| -zee | old (living beings) |
| -zima | whole, complete |
| -zito | heavy |
| -zuri | good, nice, fine, beautiful, pleasant |

II PREFIX - DEPENDENT ADJEECTIVES

| | |
|----------|--------------------------------------|
| -aminifu | honest, faithful, trustworthy |
| -ema | good, kind (in character) |
| -embamba | thin, slender, narrow |
| -ekundu | red |
| -epesi | light (in weight) quick, agile, fast |
| -erevu | clever, cunning (same as "janja") |
| -eupe | White |
| -eusi | black, dark |
| -ingi | many, much |
| -ingine | another, others |
| -ororo | soft, tender |
| -ovu | evil |

III PREFIX - INDEPENDENT ADJECTIVES

| | |
|-------------------|--|
| bora | excellent, better, best, of high quality |
| dhaifu | weak |
| ghali | expensive |
| haba | a little, few |
| halali | lawful |
| huru | free |
| hodari | efficient, able, active, strong, clever |
| kamili | exact, complete |
| laini | soft, tender (same as "ororo") |
| imara | firm, strong |
| hafifu | weak, poor, feeble |
| kadha wa kadha | several, an uncertain number |
| kila | each, every |
| gani? | what kind of? what sort of? |
| maridadi/malidadi | fancy, adorned, / beautiful |
| maskini | poor |
| maarufu | famous, well-known |
| mashuuri | important urgent |
| nadhifu | tidy, neat |
| safi | clean |
| tajiri | rich, wealthy |
| shujaa | brave, courageous |
| sita | six |
| saba | seven |
| tisa | nine |
| rahisi | easy, cheap |
| tofauti | different |
| mbalimbali | different/various |

NOTE:

The adjectival agreements or prefixes are usually the same in form as the noun prefixes, they are used to bring the adjectival stems into agreement with the nouns, as in the following examples:

| | | |
|------------------|---|------------------|
| M-toto m-dogo | - | a little child. |
| Wa-toto wa-dogo | | little children. |
| M-ti m-refu | | a tall tree. |
| Ki-su ki-kali | | a sharp knife. |
| Vi-su vi-kali | | sharp knives. |
| Chumba ki-chafu | | a dirty room. |
| Vy-umba vi-chafu | | dirty rooms. |

ZOEZI LA KWANZA - EXERCISE ONE:

COMPLETE THE SENTENCES BY INSERTING THE CORRECT FORM OF AGREEMENT

For Example: Mji wa Naivasha ni mdogo sana.

ZOEZI LA KWANZA - EXERCISE ONE

1. Nairobi ni mji _____ (kubwa).
2. Mbwa wangu ni _____ (kali) sana.
3. Ninataka kitabu _____ (ingine) _____ (pya).
4. Wadudu _____ (ingi) wanaingia nyumbani.
5. Maji ya machungwa ni kinywaji _____ (tamu).

6. Wageni _____ (ingine) wanakuja sasa.
7. Hawa ni watu _____ (zima) si watoto.
8. Minazi ni miti _____ (refu) sana.
9. Wafanyi biashara hawa ni _____ (janja) sana.
10. Ninataka mwavuli _____ (ekundu).
11. Paka wako ni _____ (eupe) si _____ (eusi).
12. Tunataka viti _____ (ingine) _____ (tatu).
13. Twiga ni mnyama _____ (refu) sana.
14. Kijana huyu anavaa viatu _____ (eusi).
15. Ngombe huyu ni _____ (nono) sana.
16. Mtumishi wangu ni _____ (refu) na _____ (embamba).
17. Mbuzi _____ (wili) _____ (eupe) wanakula majani.
18. Kiongozi _____ (ingine) atakuja.
19. Vitabu hivi ni _____ (kukuu,) si _____ (pya).
20. Chakula hiki ni _____ (zuri) sana.

ZOEZI LA PILI - EXERCISE TWO:

SAY THE FOLLOWING SENTENCES IN KISWAHILI

- a) How many loaves of bread do you want?
- b) Many visitors are coming, we need many loaves of bread.
- c) This is not my cat; my cat is black.
- d) I want two new handkerchiefs.
- e) Your (singular) new servant is lazy.
- f) These onion are nice but they are expensive.
- g) Can you (singular) bring another basket?
- h) I am giving them orange juice. Children like sweet drinks.
- i) His house is very nice.
- j) Their office has very many books.

ZOEZI LA TATU - EXERCISE 3

JIBU MASWALI HAYA - (READ THE PASSAGE IN PAGE 93 AND ANSWER THE FOLLOWING QUESTIONS)

1. Katika Kenya kuna majira gani?
2. Katika majira ya kiangazi kuna nini?
3. Majira ya masika huanza mwezi gani katika Kenya?
4. Wakulima hufanya nini wakati wa majira ya masika?
